# KARIBUNI SHULE YA CHEKECHEA YA  LARVIK

Katika kijikaratasi hiki  *utapata taarifa fupi kuhusu shule ya chekechea, na kidogo kuhusu kile mtakachokutana nacho kama watoto na wazazi katika shule ya chekechea. Shule ya chekechea ni mahali pa ustawi, urafiki, utunzaji na maendeleo. Karibu watoto wote kabla ya umri wa shule nchini Norway huhudhuria shule ya chekechea. Shughuli zote katika shule za chekechea zinasimamiwa na Sheria ya shule ya chekechea..*

Kucheza na kujifunza

Watoto watapata furaha ya kucheza na wengine katika shule ya chekechea. Katika mchezo, watoto hupata marafiki na kujumuishwa katika umoja wa kijamii. Kucheza na watoto wengine pia ni muhimu sana kwa maendeleo ya lugha na kujifunza lugha ya kinorweji. Chekechea  itahakikisha kwamba watoto wote wanashiriki katika kucheza.

Watoto wenye lugha mbali mbali.

Kujua lugha kadhaa ni rasilimali kubwa, kwa mtoto mwenyewe na kwa jamii. Wafanyakazi  watasaidia na kutambua lugha ya mama, ya watoto, wakati wanapokuza na kuendeleza ujuzi wa lugha ya watoto ya kinorweji. Mtoto anapojifunza lugha mbili kwa wakati mmoja, ni vyema shule ya chekechea na wazazi washirikiane, kwa mfano katika kuhakikisha kwamba wazazi na watoto wanaongea pamoja nyumbani kwa lugha ya mama/kutumia lugha ya mama kuelezea kuhusu kile ambacho watoto wamepitia chekechea. Soma zaidi kuhusu mada katika kijitabu,  Barn i flerspråklige familier ( Watoto katika familia za lugha kadhaa). Kijitabu hiki kinapatikana kwa lugha nyingi, kwa maandishi na pia sauti.

Utaratibu wa kazi katika shule ya chekechea

Shule zote za chekechea zina utaratibu wa kila mwaka ambao wazazi hupokea. Utaratibu wa kila mwaka umeandaliwa kwa msingi wa mpango wa kitaifa wa chekechea: Utaratibu wa mfumo wa chekechea. Mipango ya kila wiki na ya kila mwezi pia hufanywa. Mipango hiyo inaelezea jinsi shule ya chekechea inavyofanya kazi ili kuwapa watoto usalama na utunzaji, na jinsi wanavyotekeleza michezo na mafunzo. Shule zote za chekechea zina wafanyakazi ambao wana elimu inayohakikisha kuwa watoto wanapata huduma nzuri za chekechea.

Wajibu wa usiri

Wafanyakazi wa shule ya chekechea wana wajibu wa usiri. Hii ina maana kwamba wafanyakazi hawawezi kusambaza habari za kisiri kuhusu watoto, familia na wafanyakazi wenzao. Uvunjaji wa wajibu wa usiri ni kosa la jinai. Wafanyakazi wote lazima wawasilishe cheti cha rekodi ya uhalifu kabla ya kuanza kufanya kazi katika shule ya chekechea.

Ushirikiano kati ya wazazi na chekechea

Shule ya chekechea inahusika na ushirikiano mzuri baina yake na wazazi. Shule ya chekechea ingependa sana kujua ni kitu gani wazazi wanafikiria ni muhimu kwa watoto wao. Mazungumzo ya kila siku wakati wa kumleta na kumchukua ni muhimu. Zaidi ya hio, shule ya chekechea ina mikutano mbalimbali ambapo taarifa hutolewa kuhusu maudhui ya chekechea na mbinu za kufanya kazi. Baadhi ya mikutano ni ya wazazi wote kwa jumla, na mingine, ni ya mazungumzo ya kibinafsi na wazazi wa kila mtoto. Katika mikutano kama hiyo, wazazi wanaweza kutoa maoni yao kuhusu kazi katika shule ya chekechea.

Ni vizuri kama wafanyakazi na wazazi wana muda wa kuzungumza kuhusu jinsi siku imekuwa kwa mtoto katika chekechea. Unahimizwa usisite kuuliza wakati wowote una maswali yoyote.

Mkalimani

Shule ya chekechea inaweza kuagiza mkalimani kupitia huduma ya lugha. Inaweza kuwa muhimu kutumia mkalimani ili wafanyikazi na wazazi wawezea kuhakikisha kwamba wameelewana vizuri.

Nguo na vifaa

Watoto na watu wazima huwa nje kwa muda kila siku mwaka wote, na wanahitaji nguo zinazofaa kwa kila aina ya hali ya hewa. Kila mtoto anapatiwa rafu yake mwenyewe katika kabati la nguo ambamo wanaweza kuweka nguo zao wenyewe. Soma zaidi kuhusu mavazi katika msimu wa baridi kwa lugha kadhaa kwenye tovuti morsmal.no.

Chakula

Katika baadhi ya shule za chekechea, watoto huleta chakula chao wenyewe. Katika shule zingine za chekechea, chakula hutengenezwa shuleni. Wao hutumia hasa mikate, matunda na mboga. Wazazi wanalipa kiasi kidogo cha pesa kwa hili. Toa ujumbe kwa chekechea ikiwa mtoto wako ana mzio, au kama kuna vyakula ambavyo mtoto wako hapaswi kula kwa sababu ya dini.

Sherehe ya Siku ya Kuzaliwa

Ni mila kwamba wafanyakazi wa shule ya chekechea huadhimisha siku ya kuzaliwa ya mtoto. Jinsi hii inavyofanywa hutofautiana kutoka chekechea hadi chekechea. Watoto hufurahia sana wakifanyiwa sherehe ya kuzaliwa katika shule ya chekechea.

Malipo

Unaweza kuwa na haki ya kupunguziwa kwa malipo au nafasi ya kushiriki bila malipo. Kuna habari zaidi kuhusu hili kwenye tovuti ya manispaa:
https://www.larvik.kommune.no/barnehage/pris-og-redusert-betaling/

Muhimu: Maombi ya kupunguziwa malipo ni lazima yawasilishwe kabla ya tarehe 01.07. kabla ya mwaka mpya wa shule ya chekechea kuanza.

Uanzaji

Mtoto anapoanza shule ya chekechea, mmoja wa wazazi anashiriki kwa siku chache za kwanza. Baadhi ya waajiri huwapa wazazi muda wa kupumzika kutoka kazini na mshahara ili washiriki. Unakubaliana na kiongozi wa elimu katika chekechea kuhusu ni muda gani unapaswa kuwepo katika chekechea ili mtoto wako aweze kujihisi salama.

